



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2021/22

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2021



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2021/22

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2021



Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Kifungu cha 21(3) hadi (6), Sura ya 197, Benki Kuu inatakiwa kutoa Tamko la Sera ya Fedha mwanzoni mwa mwaka wa fedha, ikifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka ambayo huonesha maendeleo katika utekelezaji wa sera ya fedha. Tamko hili la sera ya fedha linajumuisha mapitio ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania, zikiwepo changamoto zinazotokana na athari za ugonjwa unaosababishwa na virusi vya *Corona (COVID-19)* katika uchumi. Pia, tamko linatoa tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo kwa mwaka 2020/21. Vilevile, tamko linaainisha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa ndani na kuweka malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2021/22, pamoja na hatua ambazo Benki Kuu itachukua ili kutimiza malengo yake kuendana na malengo ya kiuchumi ya Serikali.

Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliingia kwenye mdororo mwaka 2020, kutokana na athari za ugonjwa wa *COVID-19*. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria uchumi wa dunia kupungua kwa asilimia 3.3 (ukuaji hasi) mwaka 2020, na Benki ya Dunia ikikadiria uchumi kupungua kwa asilimia 4.3, wakati nchi chache duniani zikiiepuka mdororo wa uchumi. Nchi zilizoathirika zaidi na mdororo huu ni zile ambazo zinategemea shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa kiwango kikubwa, pamoja na zile zenye uwezo mdogo katika kukabiliana na majanga. Shughuli za biashara na uwekezaji duniani



ziliathirika zaidi mwaka 2020, kutokana na hatua zilizochukuliwa na nchi mbalimbali katika kuzuia kuenea kwa janga la *COVID-19*. Wakati huo huo, bei za bidhaa zilipungua isipokuwa bei ya dhahabu.

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika katika mwaka 2021 na hali hiyo inatarajiwa kuendelea kwa miaka ya baadaye kufuatia hatua wezeshi za sera ya fedha na bajeti katika kuongeza ukwasi, matarajio chanya ya upatikanaji na usambazaji wa chanjo za ugonjwa wa *COVID-19*, na kuanza kufunguka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2021 na asilimia 4.4 mwaka 2022, wakati Benki ya dunia inakadiria ukuaji wa asilimia 4.0 na asilimia 3.8, kwa mtiririko huo. Uchumi wa mataifa yaliyoendelea unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.1, wakati uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.7 kufuatia matarajio ya ukuaji mkubwa katika nchi za China na India. Uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 mwaka 2021, na kuongezeka hadi kufikia ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2022 kufuatia matarajio ya kuimarika kwa shughuli za kiuchumi duniani.

Mfumuko wa bei ulibakia katika viwango vya chini katika nchi nyingi japo uliongezeka kidogo katika baadhi ya nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kukua kiuchumi. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Ulaya ulikuwa wastani wa asilimia 0.4, ukipungua kutoka wastani wa asilimia 0.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20, licha



ya kuongezeka katika baadhi ya nchi hususan Ufaransa, Italia na Ujerumani. Mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) umeendelea kubakia katika kiwango kilichokubalika cha chini ya asilimia 8.0, ikiwa ni wastani wa asilimia 4.6 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021 ukilinganisha na asilimia 4.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20, kutokana na ongezeko la bei za vyakula. Katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), viwango vya mfumuko wa bei vilitofutiana baina ya nchi wanachama na kubaki ndani ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 3-7, isipokuwa kwa nchi chache.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria viwango vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea kuongezeka kidogo kufikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2021, kutoka asilimia 0.7 mwaka 2020, kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei za nishati. Wakati huohuo, mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea unatarajiwa kupungua kidogo hadi kufikia wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2021, kutoka asilimia 5.1 mwaka 2020 kutokana na kupungua kwa bei za vyakula. Vilevile, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara hadi kufikia asilimia 9.8 mwaka 2021, kutoka asilimia 10.8 mwaka 2020.



Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Tanzania Bara

Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.8 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2019 na 2018, na wastani wa asilimia 6.8 kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari hasi za ugonjwa wa *COVID-19* katika baadhi ya shughuli za kiuchumi, hususan zinazohusiana na utalii. Hata hivyo, athari za ugonjwa huu hazikuwa kubwa sana ikilinganishwa na nchi nyingine kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na ugonjwa huu, ikiwemo maamuzi ya kutofungia shughuli za uzalishaji mali. Shughuli za ujenzi zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi (asilimia 27.5), zikifuatiwa na kilimo (asilimia 25.8), usafiri na uhifadhi (asilimia 13.6) na shughuli za uzalishaji viwandani (asilimia 7.8). Aidha, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na ujenzi (asilimia 9.1), usafirishaji na uhifadhi (asilimia 8.4), na shughuli za habari na mawasiliano (asilimia 8.4).

Uchumi unatarajiwa kuimarika na kukua kwa asilimia 5.6 katika mwaka 2021, ukichangiwa zaidi na shughuli za kilimo kutokana na matarajio ya hali nzuri ya hewa, ujenzi na uchukuzi. Aidha, mazingira wezeshi ya sera ya fedha na bajeti, pamoja na utekelezaji wa maboresho na mageuzi ya kisera katika kuongeza uwazi katika kufanya biashara ukichangiwa na matarajio ya kuimarika kwa shughuli za kibiashara na uwekezaji duniani kutachangia ukuaji huu.



Mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa tulivu kuendana na malengo ya kitaifa na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa kikanda. Kwa kiasi kikubwa, kasi ndogo ya mfumuko wa bei ilichangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, uthabiti wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sera madhubuti za fedha na bajeti. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, mfumuko wa bei wa jumla ulikuwa wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kiwango cha chini kabisa cha mfumuko wa bei cha asilimia 3.0 kilirekodiwa mwezi Novemba 2020, wakati kiwango cha juu cha asilimia 3.5 kilirekodiwa mwezi Januari 2021. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisa bei za chakula na nishati, ambao unabeba sehemu kubwa katika fahirisi za bei za bidhaa, ulikuwa wastani wa asilimia 3.0 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 2.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Mfumuko wa bei za chakula ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5 hadi asilimia 3. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3 hadi 5 katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2020/21 na mwaka 2021/22 kutokana na matarajio mazuri ya upatikanaji wa chakula cha kutosha, uthabiti wa shilingi dhidi ya dola ya Marekani, pamoja na usimamizi na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

Utekelezaji wa sera ya fedha wezeshi inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi umeendelea kuchangia ukuaji wa ujazi wa fedha na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, japo kwa kasi ndogo ikilinganishwa na malengo ya mwaka 2020/21. Hali hii ilisababishwa na kupungua



kwa mahitaji ya shughuli za biashara na uwekezaji kulikotokana na athari za ugonjwa wa *COVID-19*, ambao madhara yake yalionekana zaidi kwenye shughuli zenye muingiliano wa karibu na nchi za nje. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 6.8 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10.0 na wastani wa asilimia 9.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa wastani wa asilimia 8.9 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 11.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Wastani wa fedha taslim ulikua kwa asilimia 2.8 ukilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 9.5, na ukuaji wa wastani wa asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 11.6, na wastani wa asilimia 8.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya mikopo mipya, hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na madhara ya ugonjwa wa *COVID-19* katika shughuli za biashara na uwekezaji. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuongezeka mwaka 2021/22 kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi, sera madhubuti ya bajeti na jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Vilevile, kufunguka kwa shughuli za kiuchumi katika nchi washirika wa kibiashara kunakoambatana na utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa *COVID-19*, kutaboresha zaidi ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.



Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, makusanyo ya mapato ya Serikali yalikuwa ya kuridhisha, licha ya kudorora kwa shughuli za kiuchumi duniani na athari zake katika uchumi wa ndani kulikosababishwa na *COVID-19*. Mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 16,973.0 sawa na asilimia 86 ya lengo, ikiwa ni asilimia 5.6 zaidi ya makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Mwenendo huu umetokana na kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ulioteklezwa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na ukuaji wa kuridhisha wa uchumi. Matumizi ya Serikali yameendelea kuoanishwa na kiwango cha makusanyo ya mapato, na kipaumbele kikielekezwa katika kugharamia shughuli za jamii na miradi yenye kulenga kuongeza tija kwenye uchumi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya afya, maji na elimu. Jumla ya matumizi yote ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 19,875.0, ikiwa ni asilimia 82.7 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 11,713.4 na matumizi ya maendeleo yalikuwa ni shilingi bilioni 8,161.6. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, deni la taifa limeendelea kuwa katika kiwango himilivu, kufikia dola za Marekani milioni 31,986.7, ikiwa ni ongezeko la dola milioni 2,277.8 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwezi Juni 2020. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali la ndani na nje lilikuwa dola za Marekani milioni 26,469.8 kutoka dola za Marekani milioni 24,553.3 mwezi Juni 2020, huku deni la Serikali la nje likiwa sawa na asilimia 71.6.



Sekta ya nje imeendelea kuimarika, licha ya changamoto zinazotokana na athari za ugonjwa wa *COVID-19*. Athari za ugonjwa huu kwa Tanzania hazikuwa kubwa sana kutokana na uchumi wa nchi kutegemea shughuli mbalimbali za uzalishaji, pamoja na kiwango kidogo cha uwazi katika masoko ya fedha na mitaji. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, urari wa malipo nje ya nchi ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 141.6 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 903.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Hali hii ilisababishwa na kupungua kwa fedha za washirika wa maendeleo kutoka nje ya nchi. Aidha, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje iliongezeka kidogo kufikia dola za Marekani milioni 1,072.3 kutoka dola milioni 1,000.8 kufuatia kupungua kwa mapato yatokanayo na mauzo ya huduma nje ya nchi.

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 4,969.7 kutoka dola za Marekani milioni 5,184.7 mwezi Juni 2020. Akiba hiyo inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 5.8 kiwango ambacho ni juu ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua minne.

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka na kuimarisha sekta ya benki



dhidi ya misukosuko ya ndani na nje. Aidha, ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika, kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kwenye mikopo yote kufikia asilimia 9.81 mwezi Aprili 2021 kutoka asilimia 10.84 mwezi Juni 2020. Wakati huo, Benki Kuu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kufikia kiwango kinachokubalika na Benki kisichozidi asilimia 5.0. Hatua hizo ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi zote za fedha kutumia kanzidata ya taarifa ya historia za wakopaji katika mchakato wa kutoa mikopo mipya. Pia, Benki Kuu inafuatilia na kuhakikisha kuwa benki zinatekeleza mikakati ambayo zimeainisha kwa ajili ya kupunguza mikopo chechefu. Vilevile, benki zinatakiwa kuwasilisha taarifa zao za mikopo kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji pamoja na kuwataka watumishi wa benki zote kufuata maadili ya kiutendaji yaliyoainishwa na Chama cha Mabenki Tanzania (*Tanzania Bankers Association Code of Conduct*).

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiakisi ongezeko la matumizi ya njia za kidigitali katika kufanya miamala kwa gharama nafuu. Hatua kubwa imefikiwa katika kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha ikichagizwa zaidi na matumizi ya simu za mkononi. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, idadi ya watu wazima walioweza kufikiwa na huduma za kifedha kupitia simu zao za mkononi ilifikia asilimia 78.8 ikilinganishwa na asilimia 76.2 kwa mwaka 2019/20. Mafanikio haya yalitokana na maendeleo ya kiteknolojia, ubunifu katika utoaji wa huduma za kifedha, pamoja na uwepo wa sera na mifumo madhubuti ya kiusimamizi. Matumizi



ya simu za mkononi katika kutoa huduma za kifedha hapa nchini yamekuwa chachu ya utoaji wa huduma jumuishi za fedha kwa kuyafikia makundi yasiyofikiwa na huduma rasmi za kibenki. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi yaliongezeka kufikia asilimia 92.8 kutoka asilimia 81.2 mwaka 2019/20. Ongezeko hili limechangiwa pia na jitihada za Serikali katika kukusanya mapato, kulipia ankara, malipo mengine kama ada, faini kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki ya serikali (*GePG*) na utoaji wa mikopo midogomidogo kwa njia za kielektroniki. Vilevile, mabadiliko ya kisera yaliyofanywa na Benki Kuu ya kuchochea matumizi ya huduma za kifedha kwa njia za kidigitali ikiwemo kuongeza ukomo wa kiwango cha miamala kama njia mojawapo ya kupambana na athari za janga la ugonjwa wa *COVID-19*, yalipelekea ongezeko kubwa la matumizi ya huduma za fedha kidigitali. Ongezeko hili la matumizi ya mifumo ya kidigitali katika utoaji wa huduma kwa taasisi za umma na binafsi limepunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuchangia kuongezeka kwa kasi ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Pia, matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma za kifedha kama *Quick Response (QR) Code* kupitia teknolojia ya *Masterpass na MVisa* kwa wafanyabiashara yameongeza chachu ya matumizi ya huduma za fedha kidigitali. Benki Kuu itaendelea kuboresha mazingira ili kuongeza matumizi ya mifumo ya kufanya miamala kwa njia ya kidigitali katika kutoa huduma bora zaidi za fedha nchini.



Zanzibar

Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa kasi ndogo mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2019, kutokana na athari za ugonjwa wa COVID-19 katika shughuli za kiuchumi, hususan zile zinazohusiana na utalii. Kwa mwaka 2020, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 1.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2019. Hata hivyo, uchumi umeanza kuonyesha dalili za kuimarika kutokana na kuanza tena kwa shughuli za uzalishaji mali hususan katika sekta ya huduma. Vilevile, utekelezaji wa dira ya maendeleo ambayo inahusisha uwekezaji kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi (*diversification*) unatarajiwa kuongeza chachu katika ukuaji wa uchumi.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, kufikia wastani wa asilimia 1.6, ukipungua kutoka asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kiwango hicho kidogo cha mfumuko wa bei kilitokana na kushuka kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Mfumuko wa bei za vyakula ulipungua hadi wastani wa asilimia 2.6 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa hususan unga wa mahindi na mchele wa Mbeya. Mfumuko wa bei usiohusisha bidhaa za vyakula ulipungua hadi wastani wa asilimia 0.8 kutoka asilimia 2.7, kutokana na kushuka kwa bei za sementi na mafuta. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya viwango vya tarakimu moja kwa mwaka 2021/22, kutokana na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi baada ya nchi nyingi kulegeza



masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa *COVID-19*, hususan kufungia safari na shughuli mbalimbali za kiuchumi (*lockdowns*) katika nchi ambazo Zanzibar inaagiza bidhaa.

Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, mapato ya ndani ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 616.4 sawa na asilimia 69.6 ya lengo. Matokeo haya yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za ugonjwa wa *COVID-19* katika shughuli za utalii. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 537.1 sawa na asilimia 68.0 ya lengo, wakati mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 79.3 sawa na asilimia 83.3 ya lengo. Mapato ya kodi yanatarajiwa kuimarika kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuongeza usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. Wakati huohuo, jumla ya matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 797.8 sawa na asilimia 77.6 ya makadirio kwa kipindi hicho. Matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 635.5 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 162.3. Deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 902.4 mwezi Aprili 2021, kutoka shilingi bilioni 817.7 mwishoni mwa mwezi Juni 2020, kutokana na mikopo mipya.

Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 239.0 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 40.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kukua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, pamoja na kupungua kwa mapato



ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi hususan karafuu na shughuli za utalii. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 10.9 kufikia dola za Marekani milioni 391.3, hali iliyochangiwa na kuongezeka kwa uagizaji vifaa vya uchukuzi na mashine.

Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2020/21

Malengo ya sera ya fedha katika mwaka 2020/21 yalikuwa ni kuhakikisha mfumuko wa bei unabakia kuwa tulivu ndani ya wigo wa asilimia 3-5, na kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye mfumo wa kibenki kwa ajili ya kukuza uchumi na kukabiliana na athari za ugonjwa wa *COVID-19*. Utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga pia kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ongezeko la ukuaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi. Ili kutimiza haya, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.5;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 11.6; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulifanikiwa kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye mfumo wa kibenki, na hivyo kuweka mazingira wezeshi kwa utoaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya shughuli



mbalimbali za kiuchumi. Hatua hizi zimesaidia kuendeleza utulivu wa riba katika masoko ya fedha na kiwango cha kutosha cha akiba ya mablenki ndani ya Benki Kuu. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mablenki (*overnight interbank cash market interest rate*) ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.60 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.45 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Vilevile, wastani wa riba za dhamana za serikali ulipungua na kufikia asilimia 4.62 kutoka asilimia 6.26 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020. Wakati huo huo, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na sekta ya benki ulipungua, japo kwa kasi ndogo, na kufikia asilimia 16.59 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, kutoka asilimia 16.85 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20.

Aidha, Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua kadhaa katika kuboresha huduma za fedha nchini na kusaidia uchumi kujikinga dhidi ya athari za ugonjwa wa *COVID-19*. Hatua hizi zililenga kuimarisha mizania ya mablenki na taasisi za fedha ili kuziwezesha kutoa mikopo kwa gharama nafuu. Vilevile, benki na taasisi za fedha zilipewa masharti nafuu katika kusimamia na kurekebisha mikataba ya mikopo (*loan restructuring*) na kuhimizwa kushirikiana na watoa huduma za fedha kupitia simu za mkononi ili kukuza matumizi ya huduma za malipo kielektroniki. Kwa ujumla, hatua hizi zimesaidia kuimarisha ukwasi kwenye mfumo wa kibenki na kuendeleza sekta imara ya kibenki.



Sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi uliongezeka, japo kwa kasi ndogo kulinganisha na lengo la mwaka 2020/21. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3), uliongezeka kwa wastani wa asilimia 6.8 ukilinganishwa na lengo la asilimia 10.0. Wakati huo huo, wastani wa ukuaji wa fedha taslimu ulikuwa asilimia 2.8 ukilinganishwa na lengo la asilimia 9.5. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.3, dhidi ya lengo la asilimia 11.6, hali iliyosababishwa na athari za ugonjwa wa *COVID-19* katika shughuli za uwekezaji na biashara.

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu mbalimbali duniani imeendelea kuwa tulivu katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2020 hadi Aprili 2021. Mwenendo huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na utulivu wa mfumuko wa bei nchini, utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti, na mwendelezo wa nakisi ndogo katika urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje. Katika kipindi hiki, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa kati ya shilingi 2,309.0 na shilingi 2,310.0 ikilinganishwa na shilingi 2,300.0 hadi shilingi 2,302.2 kwa dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20.



Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2021/22

Mwaka 2021/22 Serikali itanza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 (*FYDP III*) ambao unatarajiwa kukamilisha malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 ya kuboresha maisha ya Watanzania na kujenga uchumi imara unaoweza kukabilliana na ushindani kutoka nchi nyingine. Baadhi ya malengo ya mpango huu ni pamoja na kukuza uchumi shindani na jumuishi, kukuza uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, kukuza biashara na kuchochea maendeleo ya rasilimali watu kwa ajili ya kuhakikisha ukuaji shirikishi wa uchumi. Katika mwaka 2021/22, Serikali inalenga kufikia malengo ya kiuchumi yafuatayo:

- i. ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 5.6 kwa mwaka 2021;
- ii. mfumuko wa bei ulio ndani ya kiwango cha tarakimu moja, kati ya wastani wa asilimia 3 hadi 5 kwa mwaka 2021/22; na
- iii. nakisi ya bajeti, ikijumuisha misaada kutoka nje (*grants*), ya asilimia 1.8 ya Pato la Taifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mwaka 2021/22.

Kwa upande wa uchumi wa Zanzibar, Serikali inalenga kufikia malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 5.2 mwaka 2021;
- ii. mfumuko wa bei ulio chini ya wastani wa asilimia 5 kwa mwaka 2021/22; na



- iii. nakisi ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ikijumuisha misaada kutoka nje (*grants*), ya asilimia 2.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/22.

Utekelezaji wa sera ya fedha utaendelea kuongozwa na malengo mapana ya Serikali ya kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi. Katika kusimamia jukumu hili, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika mfumo wa kibenki ili kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi, bila kuathiri utulivu wa mfumuko wa bei katika kiwango kinachotarajiwa. Utekelezaji wa sera hii ya fedha unatarajiwa kusaidia ongezeko la utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Ili kufikia malengo haya kwa mwaka 2021/22, Benki Kuu imepanga kufikia malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.9;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.6; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuboresha ufanisi wa masoko ya fedha ikiwa ni pamoja na miundombinu yake na kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa ajili ya kuboresha uelewa juu ya mambo muhimu katika sekta ya fedha. Pia, Benki Kuu itaendelea na jitihada za kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha kuelekea matumizi ya riba kama kiashiria cha sera ya fedha kwa ajili



ya usimamizi madhubuti wa sera ya fedha. Mfumo unaotumia riba ni bora zaidi katika kusimamia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya kiuchumi kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi na ya kiteknolojia. Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa uwazi zaidi na kwa kutumia nyenzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kulingana na mahitaji ya uchumi. Hatua hizi zinatarajiwa kuleta utulivu katika riba za muda mfupi na kusaidia kufikiwa kwa malengo ya utulivu wa mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi.

Hitimisho

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuimarika na kukua kwa asilimia 5.6 au zaidi mwaka 2021, kufuatia uwekezaji unaofanywa na Serikali katika miradi ya maendeleo, uwepo wa sera wezeshi ya fedha na bajeti, na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi itategemea kuimarika kwa biashara na uwekezaji duniani, pamoja na kupungua kwa kutotabirika kwa mwelekeo wa uchumi wa dunia kunakoambatana na ugonjwa wa *COVID-19*.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu na unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo la kati ya asilimia 3 hadi 5 kutokana na matarajio ya hali nzuri ya hewa, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi duniani. Aidha, kuna hatari ya mfumuko wa bei kupanda kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia



kulikoanza kuonekana hivi karibuni. Benki Kuu kwa upande wake itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwa kuzingatia utulivu wa mfumuko wa bei, na itakuwa tayari kuchukua hatua za ziada endapo kutakuwa na dalili za kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na Serikali katika kushughulikia changamoto zilizopo kwenye sekta ya fedha ili kusaidia katika kuweka mazingira wezeshi ya kupungua kwa viwango vya riba za mikopo na kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, na kuendeleza utulivu wa sekta ya fedha. Kutokana na matarajio ya kurejea kwa hali ya kawaida ya uchumi wa dunia na kuimarika kwa uchumi wa ndani, Benki Kuu ina matumaini kwamba malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko hili la mwaka 2021/22 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328/9, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: <http://www.bot.go.tz>